MAJI TANZANIA

TOLEO NA 019

JANUARI- MACHI, 2022

# Siku ya Maji Duniani Kitaifa Yafana, Mhe. Rais Samia Aipongeza Sekta ya Maji






Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amewataka watendaji wa sekta ya maji kuzingatia weledi na miongozo ya Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maji.

# Waharibifu wa Miundombinu ya Maji Wachukuliwe Hatua



# Siku ya Maji Duniani Kitaifa Yafana, Mhe. Rais Samia Aipongeza Sekta ya Maji




*Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akihutubia Siku ya Maji Duniani Kitaifa, Jijini Dar es salaam*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali itatoa fedha za kujenga Bwawa la Maji la Kidunda mkoani Morogoro ili kumaliza changamoto ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama Jijini Dar es Salaam na mkoa wa Pwani.

Rais Samia ametoa kauli hiyo wakati akihutubia Siku ya Maji Duniani Kitaifa Jijini Dar es Salaam katika Ukumbi wa Mikutano wa Mlimani City, na kutoa kongole kwa watendaji wa Sekta ya Maji kwa kazi wanayofanya ya kuihudumia jamii, hussani katika huduma ya majisafi na usafi wa mazingira..

Rais Samia amesema mradi huo mkubwa utawezesha upatikanaji wa uhakika wa maji kwa kipindi chote mwaka mzima kwa Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Mkoa wa Pwani kwa kuwa kwa sasa mikoa hiyo inategemea maji ya Mto Ruvu ambayo asilimia 88 ya maji yote yanayozalishwa kwa ajili ya kuhudumia wakazi wake.

Rais Samia amesema kuwa kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira uliokithiri katika chanzo cha Mto Ruvu, kina cha maji cha mto huo kimekuwa kikipungua hasa wakati wa kiangazi hivyo mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini kukosa kusukuma maji ya kutosha na kuleta changamoto ya huduma ya maji kwa wananchi.

Akisisitiza kuwa ujenzi wa bwawa hilo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2022 mpaka 2025.

Aidha, Rais Samia amezindua Mfumo wa Pamoja wa Kusimamia Ankara za Maji (Unified Billing System) na Mfumo wa Taarifa za Miradi ya Maji (Maji App) iliyotengenezwa na wataalamu wa ndani, itakayoimarisha zaidi utoaji huduma ya maji kwa wananchi.

Pamoja na hilo, ametoa tuzo kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira zilizofanya vizuri kiutendaji Tanzania Bara kutokana na Ripoti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji nchini (EWURA) kwa Mwaka 2020-2021.

Siku ya Maji Duniani, Kitaifa iliambatana pia na tukio laMhe. Rais Samia kuzindua Mradi wa Maji wa Mlandizi-Chalinze-Mboga katika Kata ya Msoga, mkoani Pwani wenye thamani ya Shilingi bilioni 19 ambao ujenzi wake ulisimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA).

Baadhi ya maeneo yanayohudumiwa na mradi huu ni mji wa Chalinze na vitongoji vya Kata ya Msoga, Viwanda vya Tywford, Sayona, Kituo cha Treni ya Mwendokasi cha Kwala, Eneo la Mizani la Vigwaza pamoja na maeneo maalumu yaliyotengwa kwa ajili ya viwanda.

Kaulimbiu ya Siku ya Maji Duniani mwaka 2022 ni Maji Chini ya Ardhi; Hazina Isiyoonekana kwa Maendeleo Endelevu. Siku hii ni moja ya matukio ya kalenda ya Umoja wa Mataifa, ambapo nchi wanachama wa umoja huo huadhimisha kila mwaka ifikapo Machi 22.

## SIKU YA MAJI DUNIANI KITAIFA, MACHI 22 KATIKA PICHA; DAR ES SALAAM -MLIMANI CITY




Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na viongozi wengine katika meza kuu, wakijumuika kwa picha ya pamoja na sehemu ya viongozi waliohudhuria Siku ya Maji Duniani Kitaifa.

Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua ripoti ya utendaji kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Maji Duniani.









Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiongea na Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), wakati wa Siku ya Maji Duniani Kitaifa, iliyofanyika Mlimani City, jijini Dar es salaam.

# Moshi Vinara wa utoaji huduma ya maji




*Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi Mhandisi Kija Limbe akiwa na tuzo baada ya Mamlaka anayoiongoza kuibuka kinara kati ya mamlaka zinazotoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira hapa nchini. Kulia ni Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga, na kushoto kabisa ni Mkurugenzi Msaidizi, Ufuatiliaji na Utoaji Huduma Mhandisi Lydia Joseph.*



*Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akitoa zawadi kwa mmoja kati ya wastaafu walioagwa, Mhandisi Joshua Mgeyekwa, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga (KASHWASA). Mhandisi Mgeyekwa anastaafu Utumishi wa Umma.*




*Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi Mhandisi Kija Limbe (kushoto) akiwa na mfano wa hundi na kiasi cha fedha ambacho mamlaka anayoiongoza imeshinda. Kulia ni Mhandisi Augusto Shoo, Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa mamlaka hiyo iliyoibuka mshindi.*

# Waharibifu wa Miradi ya Maji kuchukuliwa hatua

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango ameagiza yeyote anayekwamisha na kuhujumu miradi ya maji kuchukuliwa hatua za kisheria.

Dkt. Mpango ametoa tamko hilo katika uzinduzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Maji Kitaifa katika hafla iliyofanyika katika Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara. Makamu wa Rais Dkt. Mpango amesema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imetoa kipaumbele kwenye Sekta ya Maji kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji na haitakuwa tayari kuona miradi hiyo ikikwamishwa au kuhujumiwa na mtu yeyote.

Akizitaka mamlaka husika kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kusimamia, kuitunza na kuilinda miradi hiyo pamoja na kuwachukulia hatua kali za kisheria watu wote wenye tabia hiyo ili miradi hiyo iweze kudumu na kutoa huduma ya maji kwa muda mrefu.

Pia, Dkt. Mpango amesema kuwa ni muhimu kutunza mazingira ili kuepuka athari za mabadiliko ya tabianchi ili kuwa na vyanzo vingi na vya uhakika vya maji kwa kuwa ndio msingi wa huduma bora ya maji na ya uhakika wakati wote.

Dkt. Mpango ameipongeza Wizara ya Maji kwa kuing'arisha Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa na nzuri ya utekelezaji wa miradi ya maji maeneo mbalimbali nchini na kuahidi kuwa Serikali itaendelea kuiwezesha Wizara hiyo ili kufikia lengo yake ya kufikisha huduma ya majisafi na salama kwa asilimia 95 mijini na asilimia 85 vijijini ifikapo mwaka 2025.

Awali, Dkt. Mpango aliweka jiwe la msingi kwenye Mradi wa Maji wa Orkesumet wilayani Simanjiro wenye thamani ya Shilingi bilioni 41.5 utakaohudumia zaidi ya wakazi 52,000 na kuhudumia mifugo katika kata za Orkesumet, Langai na Edonyongijape na vijiji vya jirani na mji wa Simanjiro, ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 99 chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati (BAWASA).





*Wiki ya Maji 2022: Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Mpango na Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), pamoja na viongozi wengine, wakionyesha ishara ya furaha baada ya Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Mpango kuweka jiwe la msingi la mradi wa maji wa Orkesumet, Simanjiro.*









*Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiweka jiwe la msingi katika miradi ya maji mkoani Mara*








*Mrisho Mpoto Mjomba, Balozi wa Hiari wa Sekta ya Maji*

# Dakika 30 za Aweso: Kazi na Tuzo



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amewataka watendaji wa sekta ya maji kuzingatia weledi na miongozo ya Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maji.

Amesema kwa sasa kazi inaendelea na inaridhisha kwa mwenendo wake ila watendaji wasijisahau na kuharibu yaliyo mema.

Waziri Aweso amesema hayo leo Februari 23, 2023 aliooongea katika uzinduzi wa matokeo ya tathmini ya utendaji programu ya Lipa kwa matokeo ( Pay by Result) awamu ya 6 (PbR6) naLipa kutokakana na Matokeo, (Pay for Result awamu ya Pili (PforR2).

Aidha, Aweso ametumia dakika 30 kuendesha kikao na Menejimenti ya Wizara ya Maji, na taasisi zake ikiwamo, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mabonde ya Maji, Mamlaka za Maji na Chuo cha Maji.

"Kwa dhati ya moyo wangu niwapongeze watendaji wa sekta ya maji. Tulikotoka hali ya utekelezaji wa miradi ya maji ilikuwa mbaya, Kwa sasa kuna mabadiliko makubwa. Niwapongeze na kuwatia moyo kwamba sisi viongozi wenu tuko bega kwa bega na nyinyi." Waziri Aweso amesema.

Amempongeza Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mhandisi Clement Kivegalo kwa kutambua jitihada za watendaji wa sekta hiyo na kuwapa motisha ili kuongeza kasi ya kuwahudumia wananchi vijijini.

Amesema uamuzi wa kuanzisha RUWASA Julai 2019 umeleta tija kubwa katika sekta ya maji kwani kwa muda mfupi sana matokeo ya utendaji yameonekana. Miradi iliyokuwa imekwama kabla ya kuanzisha kwa RUWASA imekwamuliwa.

Aidha, amesisitiza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ana matumaini makubwa ya kuondoa changamoto ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa Watanzania kupitia rasilimali watu aliyo nayo ndani ya Wizara ya Maji.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amesisitiza ushirikiano katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za sekta ya Maji.
" Tuendelee kusadiana kutimiza majukumu yetu. Tufahamu kwamba sisi sote ni Wizara ya Maji bila kujali kwamba huyu ni RUWASA, huyu ni Mamlaka ya Maji au Bonde la Maji. Hakikisha kila wakati unachukua hatua mambo yote yaende vizuri" Amesema Mhandisi Mahundi

Katika tukio hilo, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Nadhifa Kemikimba amesisitiza umuhimu wa kutunza takwimu ili kuweza kufanya maamuzi yaliyosahihi katika kutoa huduma kwa Umma.

"Watumishi wa sekta ya maji mhakikisha mnakusanya, mnachakata mnahifadhi na kutoa takwimu sahihi kwa ajili ya mipango ya wizara. Eneo la Takwimu ni eneo muhim ambalo linaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kupanga mipango ya Wizara."

Kufuatia matokeo ya tathmini, Waziri Aweso ametoa zawadi kwa Watendaji mbalimbali wa RUWASA katika ngazi ya mikoa na wilaya zilizofanya vizuri katika program tofauti tofauti ambapo mkoa wa Tabora umeongoza kwa upande wa program ya PforR2 wakati Njombe ikiongoza kwa program ya PbR6

# Tanzania kufaidika zaidi kwa Utunzaji wa Rasilimalimaji



*Naibu Waziri wa Maji Mhe. Maryprisca Mahundi (Mb) akiongoza Mkutano wa kwanza wa Baraza la Mawaziri, Kamisheni ya Bonde la mto Songwe uliofanyika jijini Lilongwe, Malawi ambapo masuala ya rasilimali za maji yanayozihusu nchi za Tanzania na Malawi yamefanyiwa kazi kwa ushirikiano na wataalamu wa pande zote mbili za nchi hizo. Kushoto ni Waziri wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Malawi Mhe. Abida Sidik Mia (Mb).*



*Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) akipitia makabrasha kuhusu Mkutano Mkutano wa kwanza wa Baraza la Mawaziri, Kamisheni ya Bonde la mto Songwe Jijini Lilongwe. Wizara ya Ardhi ni moja ya wizara muhimu katika kufanikisha kazi mbalimbali za maendeleo ya wananchi katika bonde hilo.*

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Maryprisca Mahundi (Mb) amesema Tanzania inaendelea kunufaika pamoja na wananchi wake kwa kujenga uhusiano mzuri na mataifa mbalimbali, zikiwemo nchi jirani zinazoizunguka.

Mhe. Mahundi amesema hayo wakati wa Mkutano wa kwanza wa Baraza la Mawaziri, Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe uliofanyika jijini Lilongwe, Malawi.
Amesema kupitia Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe kazi inafanyika kwa ushirikiano kuondosha changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi wa Tanzania na Malawi kupitia wataalamu wa rasilimali za maji, ikiwemo ujenzi wa mabwawa katika bonde hilo ambayo itakuwa suluhu ya mafuriko yanayoharibu mali mbalimbali ikiwamo mazao kwa kujenga bwawa la Songwe Chini, na mazingira.

Aidha, kuwezesha kilimo cha umwagiliaji zaidi ya hekta 6,000 na kupata nishati ya uhakika ya umeme kwa nchi mbili kugawana megawati zipatazo 180.
Mhe. Mahundi amesema hayo ni mafanikio ya mahusiano yaliyojengwa na viongozi wa nchi mbili katika kuhakikisha wananchi wanafanya kazi kwa maendeleo ya nchi zao. Amesema kazi hiyo ni matunda ya viongozi Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mhe. Lazarus Chakwera , Rais wa Malawi.

Pamoja na hatua hiyo, amewataka wananchi kuendelea kutunza mazingira na vyanzo vya maji ili kuhakikisha huduma ya maji na miradi ya maji inakuwa endelevu na kutoshelezа mahitaji ya jamii kwa sasa na vizazi vijavyo.
Kamisheni ya Bonde la mto Songwe inaundwa kwa Pamoja na nchi za Malawi na Tanzania, ambapo katika kikao hicho Mawaziri wamekubaliana na kusaini Kanuni za uendeshaji wa vikao vya Mawaziri.

# Sekta ya Maji yaaminiwa zaidi



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Bw. Amos Cheptoo, viongozi wa Wizara ya Maji, pamoja na timu nzima ya wataalamu wa sekta ya maji iliyoshiriki kikao jijini Arusha.

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amemshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Bw. Amos Cheptoo kwa ushirikiano mkubwa unaotolewa na taasisi anayoiongoza na kuwa sehemu ya mafanikio makubwa katika Sekta ya Maji hapa nchini.

Waziri Aweso ametoa shukrani hizo na kuahidi ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maji katika kikao kilichofanyika jijini Arusha kwa lengo la kujadili maendeleo ya utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Jiji la Arusha wenye thamani ya Sh. bilioni 520 ambazo sehemu ya fedha hizo kiasi cha Dola za Marekani 210,962,581 ikiwa ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika.
Akizungumzia mafanikio yanayotarajiwa baada ya kukamilika kwa mradi huo, Mhe. Aweso amesema mradi umelenga kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira jijini Arusha na baadhi ya maeneo ya wilaya ya Arumeru na utaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 40 kwa siku mpaka lita 200 kwa siku kufikia mwaka 2030, kuongezeka wanufaika wa huduma kutoka 325,000 mpaka 1,009,548, kuongeza mtandao kutoka asilimia 44 mpaka asilimia 100 ambapo kilomita 760.4 za mabomba zitalazwa.

Pia, kuongeza mtandao wa majitaka ulio asilimia 7.6 kwa sasa mpaka asilimia 30 ambapoumbali wa kilomita 192 za mabomba ya majitaka zitalazwa na kunufaisha wananchi 201,811, ujenzi wa mtambo mpya wa kutibu majitaka wenye uwezo wa

kutibu lita milioni 22 za majitaka kwa siku pamoja na kujenga uwezo kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA) kupitia mafunzo, ununuzi wa samani za ofisi na vitendea kazi.

Katika kikao hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Bw. Amos Cheptoo amesema lengo la ujio wao ni kujionea kazi iliyofanyika ya mradi wa jiji la Arusha na wataendelea kuipa ushirikiano Tanzania ili kuhakikisha Serikali inafikia malengo yake kwa upande wa Sekta ya Maji pamoja na sekta nyingine.

Pamoja na viongozi hao, kikao hicho pia kilihudhuriwa na Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Nadhifa Kemikimba, Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, Joyce Msiru, Waratibu wa Mradi huo kutoka Wizara ya Maji pamoja na maafisa kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika.



# "2022 Maji kazi safi na mnaimarika" ~ Waziri Mkuu Majaliwa



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) akizindua Mradi wa Maji wa Mogitu-Katesh katika Mji wa Katesh, mkoani Manyara*

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) ameweka jiwe la msingi na kuzindua Mradi wa Maji wa Mogitu-Katesh katika Mji wa Katesh, Wilaya ya Hanang', mkoani Manyara.

Waziri Mkuu Majaliwa ameshiriki hafla hiyo baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza ya mradi huo iliyogharimu ya Sh. bilioni 2.5 uliotekelezwa na Kampuni ya Mtembesha chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati (BAWASA).

"Nampongeza Waziri wa Maji, Jumaa Aweso na Wizara ya Maji kwa ujumla kwa kazi nzuri mliyoifanya hapa Katesh. Tunazidi kuona mafanikio makubwa kwenye Sekta ya Maji na huduma ya majisafi na salama ikizidi kuimarika katika maeneo mbalimbali nchini", amesema Waziri Mkuu Majaliwa.

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema mradi huo unatekelezwa kwa awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza imekamilika na baada ya kukamilika kwa awamu hiyo baadhi ya wananchi wameanza kupata huduma ya majisafi na salama na kuongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 45.2 hadi kufikia 56.8 mwezi, Disemba, 2021.

Akiongeza kuwa mradi utakapokamilika utazalisha lita milioni 2.5 za maji kwa siku na kunufaisha wananchi wa mji mdogo wa Katesh na vijiji vya jirani.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati (BAWASA), Mhandisi Iddy Msuya amesema tayari utaratibu wa utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi umeanza na wameshapokea fedha kutoka wizarani kwa ajili ya kuanza kazi hiyo.

Awamu ya pili ya mradi huo itagharimu Sh. bilioni 2.3 kwa utekelezaji wa kazi za kuondoa miundombinu chakavu na kupeleka huduma ya maji katika kwenye kata za Jorodom, Ganana, Dumbeta na Katesh na mradi wote unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Disemba, 2022 ukiwa na thamani ya Sh. bilioni 4.8.



# Haduma ya majisafi kuwafikia wananchi kila kona

Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) akizindua mradi wa maji wa Maghang-Maghang Juu – Gidimadoy , wilaya ya Mbulu mkoani Manyara. Mhe. Majaliwa katika uzinduzi huo amewahakikishia wananchi Serikali imeweka mkakati mahsusi kumaliza uhaba wa majisafi kwa wananchi.



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiongea katika uzinduzi huo ameema serikali imetega kiasi cha shilingi bilioni 16 zitakazotumika katika ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji mkoani Manyara.



# Ni Jibondo, Mafia - maji yapitishwa chini ya bahari





*Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akizindua mradi wa maji katika kisiwa cha Jibondo, Mafia. Moja ya sifa ya mradi huu kupitia kazi iliyofanywa na wataalam wa maji ni mabomba ya majisafi kupita chini ya bahari kwa umbali wa kilomita 7.8.*

Kitengo cha Mawasiliano

Tovuti: www.maji.go.tz